

## **Changamoto za Kutafsiri Vihisishi katika Matini: Mifano kutoka Matini za Kifasihi**

na

Juma Hashim

*“Makala hii naitabaruku kwa rafiki yangu kipenzi Philemon Anthony Roman, alifariki dunia kwa ajili ya moto tarehe 28/12/2021. Natambua mchango wake kwenye taaluma ndio maana nimeamua nimuandikie makala hii. Kila nafsi itaonja umauti, Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi Amin”.*

### *Ikisiri*

*Vihisishi ni maneno ambayo hubeba hisia kama vile mshangao, furaha na huzuni. Aidha, Nyangeri (2016) anaeleza kuwa vihisishi ni kundi la maneno ambalo hupewa jukumu la pembeni na wasomi wakiwemo wafasiri. Hata hivyo, kundi hili la maneno lina nafasi kubwa sana katika kufanikisha mawasiliano katika tafsiri. Kutokana na maelezo hayo tumebaini kuwa kama kundi hili la maneno lina nafasi kubwa katika kufanikisha mawasiliano katika tafsiri, je kundi hili la maneno linakumbana na changamoto zipi wakati wa kuvitafsiri? Swali hilo ndilo limepelekea makala haya yachunguze changamoto za kutafsiri vihisishia. Hivyo basi, makala haya yamechunguza changamoto ambazo zimejitokeza wakati wa kuvifasili vihisishi kama maneno ambayo hutumika kufanikisha mawasiliano katika tafsiri. Aidha, makala haya yameanzia tamthilia ya Kinjekitile iloyoandikwa na Hussein (1969a) na tafsiri yake ya kiingereza (1969b) na Tamthilia ya Amezidi ya Mohamed, 1995 na tafsiri yake ya ‘He is Far Too Much’ (Wafasiri Weschler na Kimambo, 2012). Pia, makala haya yameanza kwa kuangalia dhana ya vihisishi, matini na kisha changamoto za kutafsiri vihisishi katika matini za kifasihi.*

### **1.0 Utangulizi**

Vihisishi ni maneno ambayo hubeba hisia kama vile mshangao, furaha na huzuni. Hisia hizo zaweza kuwa furaha, huzuni, hasira, kinyume na matarajio, kushituka, woga na kadhalika (TUKI, 2013; BAKITA, 2015). Kihisishi kwa kawaida katika maandishi hutambuliwa kwa kufuatwa na alama ya hisi (!) au mshangao. Pia, makala haya yameangazia aina kuu mbili za vihisishi, aina hizo ni vihisishi asilia, mfano Aaaah! oooh! na vihisishi visivyo asilia mfano neno Bwana!.

Aidha, kuhusu dhana ya matini wataalamu kadhaa wanafasili dhana hiyo, miongoni mwao ni Massamba (2009) anaeleza kuwa matini ni maelezo ya kitu ambayo ama yameandikwa na mtu au yamenukuliwa na ambayo yamekusudiwa kutumiwa kwa makusudi maalumu. Pia, TUKI (2013) wanaeleza kuwa matini ni maelezo kuhusu jambo lolote lile ambalo limeandikwa au kunakiliwa. Kutokana na fasili za wataalamu hao tunabaini kuwa kuna masuala kadhaa ambayo yanaibuka kutokana na fasili zao, miongoni mwa mambo hayo ni; mosi, matini huweza kuandikwa au kunukuliwa. Pili, matini hutumiwa kwa lengo maalumu. Kutokana na mambo hayo tunaweza kuhitimisha kwamba, matini ni maelezo ya kitu au jambo ambayo huweza kuandikwa au kunukuliwa ili kutumika kwa lengo maalumu.

Kwa upande wa matini za kifasihi, Mwansoko na Wenzake (2013) wanasema kuwa matini za kifasihi ni matini ambazo huandikwa kwa lengo la kunufaisha nafsi ya msomaji kwa kutumia sanaa ya lugha na mfasili hanabudi kuwa sehemu ya mwanalugha husika kama atahitaji kuifasili matini ya kifasihi. Kutokana na maelezo hayo, tumehitimisha kuwa, matini ya kifasihi ni aina ya matini ambayo huwa na sanaa ya lugha ambayo mwandishi huwa na wazo fulani ambapo anakuwa na hamu ya kukonga moyo wake kuiandikia hadhira anayoikusudia. Baada ya kutazama maana ya vihisishi, matini na matini za kifasihi sehemu inayofata tumeangalia changamoto za kutafsiri vihisishi katika matini mbalimbali za kifasihi. Hebu sasa tutazame changamoto hizo katika sehemu inayofata.

## **2.0 Changamoto za Kutafsiri Vihisishi katika Matini Mbalimbali za Kifasihi**

Katika kipengele hiki tumeangazia changamoto mbalimbali za kutafsiri vihisishi, changamoto hizi huwa zinaibuka endapo mfasiri asipovizingatia vihisishi katika uhawilishaji wake na kupelekea kuibua changamoto kadhaa. Hivyo basi, changamoto hizo zimebainishwa kama ifuatavyo:

### **2.1 Kutumia Kihisishi chenye Maana tofauti na Matini Chanzi**

Wafasiri hutumia vihisishi vyenye maana tofauti na ile ya matini chanzi. Matini chanzi huweza kubeba kihisishi kinachodokeza furaha, huzuni, mshangao lakini mfasiri akatumia kihisishi chenye maana tofauti na ile iliyobebwa kwenye matini chanzi. Hebu tutazame mfano wa 1 kutoka katika tamthilia ya *Amezidi*.

Mfano wa 1

•**Matini Chanzi:** Ame: Nini bwana!

•**Matini Lengwa:** Heezfar: What man!

Chanzo: Mohamed, (2012:4)

Katika mfano wa 1 hapo juu tunaona kuwa kumefanyika tafsiri kutoka lugha chanzi na kwenda lugha lengwa. Kihisishi 'bwana' katika matini chanzi kinalipa neno hili maana tofauti na ile ya kikamusi ambayo imezingatiwa katika tafsiri. Tungo 'nini bwana' katika muktadha huo huwasilishwa kupitia ishara zisizo za kiisimu kama vile mkazo, kidatu pamoja mwonekano wa uso. Katika tamthilia ya *Amezidi* mhusika 'Ame' alikuwa katika hali ya kisaikolojia ya kuchukizwa hali ambayo haijajitokeza waziwazi katika tafsiri inayotolewa hapo kwenye mfano wa kwanza. Kuna kipengele cha kejeli katika tamko la 'Ame' ambalo ni (nini bwana!). Hivyo basi, tafsiri ambayo ingefaa zaidi kutolewa na mfasiri labda ingekuwa "Mr! What is it?".

## 2.2 Wafasiri Kubadilisha Kihisishi

Hii ni changamoto nyingine inayojitokeza katika kufasiri vihisishi kutoka katika lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Baadhi wafasiri wanapokutana na vihisishi katika matini zao huvibadilisha jambo ambalo hupelekea kukosa maana kama ilivyokusudiwa. Hebu tutazame mfano wa 2 kwa ufafanuzi zaidi.

Mfano wa 2

### •**Matini Chanzi**

Zidi: Aha...umesema mhogo uliovunda?

Ame: Mhogo uliovunda? nani kasema mhogo uliovunda au una njaa?

Zidi: Mhogo uliovunda enh!

Ame: Mhogo tokea lini kvunda?

Zidi: Ah, (anafanya kukumbuka kitu) kweli mhogo hauvundi.

### •**Matini Lengwa**

Tumach: Ah, so you are saying, the cassava that moulded?

Heezfar: The cassava that moulded”? Who mentioned anything about a cassava moulding? Are you hungry or something?

Tumach: enh, the cassava that moulded?

Heezfar: Since when does cassava mould?

Tumach: Ah! (pretends to have suddenly remembered something) of course

Chanzo: Mohamed, (2012:5)

Katika mfano wa 2 hapo juu, tunaona kuwa kuna kihisishi ‘Aha’ katika matini chanzi ambayo hutumika kuashiria utambuzi wa ghafla. Msemaji anaelewa kwa ghafla kitu, tukio, jambo au hali ambayo awali hakuielewa (taz: Wamitila 2003). Hata hivyo, kihisishi kilichotumika katika matini lengwa ni ‘ah’ ambacho hutumika kuashiria mshangao, furaha, pongezi, huruma kuchanganyikiwa au msemaji kutokukubaliana na jambo. Kwa hiyo, mfasiri ameamua kutumia kihisishi kingine chenye maana tofauti na kihisishi cha awali. Kwani mhusika ‘Zidi’ alilenga kuwasilisha furaha aliyonayo kuwa ameelewa ujumbe wa mhusika ‘Ame’ kuwa anarejelea ‘mhogo uliovunda’ basi kihisishi sahihi kingekuwa Aha!

### **2.3 Wafasiri Kuongeza Maelezo wakati wa Kukielezea Kihisishi**

Wafasiri wa matini za kifasiri hujikuta wanatumia maelezo wakati wa kuvifasili vihisishi kutoka katika lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Katika tamthilia ya *Kinjikitile* ya Hussein, (1969b) mfasiri ameingiza maelezo ya ishara wakati wa ufafanuzi wa kihisishi. Suala hili linajidhihirisha katika ukurasa wa 11 katika tamthilia hiyo ya *Kinjikitile*. Hebu tutazame mfano wa 3 kwa uthibitisho zaidi.

Mfano wa 3

•Matini Chanzi- Bibi 1: Na yeye hakutamani (wanacheka)- Matini Chanzi

•Matini Lengwa- First Woman: Ah, so she doesn’t turn toward you! (she laughs mischievously)

Chanzo: Hussein (1969:11)

Katika mfano wa 3 hapo juu tunaona kuwa katika matini lengwa tafsiri iliyotolewa imeongezewa kihisishi cha kuwasilisha hisia za furaha ambazo zimewasilishwa kupitia maelezo yaliyomo.

Aidha, kihisishi ‘Ah’ kilichoongezwa katika matini lengwa kimechochewa na muktadha wa mawasiliano uliomo katika matini chanzi. Lengo hasa likiwa na kubainisha hisia ya furaha ambazo zimewasilishwa kupitia maelezo yaliyomo.

#### **2.4 Mara nyingine Wafasiri Huamisha Kihisishi kama kilivyo wakati wa Kutafsiri Matini Chanzi-Matini Lengwa**

Mfasiri anapohawilisha mawazo kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa ni sharti atafute visawe vya maneno husika ili vimsaidie wakati akiwa anahawilisha mawazo hayo. Hata hivyo, kuna baadhi ya mazingira humfanya mfasiri ahamishe neno kutoka kwenye lugha chanzi na kulipeleka kwenye lugha lengwa kama lilivyo. Hebu tatazame mfano wa 4 kwa ufafanuzi zaidi.

Mfano wa 4

- Matini Chanzi: “Hodi! Hodi! fungua mlango
- Matini Lengwa: “Hodi! Hodi! open the door

Chanzo: Hussein, (2012:8)

Katika mfano wa 4 hapo juu tunaona kuwa tafsiri iliyotolewa imehamisha kihisishi ‘hodi hodi’ kama kilivyo kutoka katika lugha chanzi bila kutoa maelezo yoyote ili kumwezesha msomaji wa matini lengwa kuelewa matumizi yake. Hata hivyo, hali hii husababishwa na mfasiri kukosa kisawe muafaka kinachoendana na kihisishi ‘hodi’ na kupelekea kukiamisha kama kilivyo kwenye matini lengwa. Hivyo, visawe vinavyopendekezwa kulingana na kihisishi ‘hodi’ ni ‘hey’ na ‘hallo’ visawe hivi ni muafaka zaidi kutumika zaidi kama mbadala wa kihisishi hodi!

### **3.0 Hitimisho**

Makala haya yameanza kwa kuangazia maana ya vihisishi na matini katika upande wa utangulizi. Makala haya yameangazia changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wa kuvitafsiri vihisishi. Changamoto hizo zimebainishwa katika kipengele cha (2.0) katika makala haya. Pia, mwandishi wa makala haya amependekeza kuwa mbinu ya kimawasiliano itumike wakati wa kuvitafsiri vihisishi kwani vihisishi mara nyingi hufungamana na muktadha wa jamii. Aidha, Mwandishi wa makala haya amependekeza kuwa mfasiri anapokuwa anatafsiri vihisishi ni lazima atambue kwamba kutafsiri vihisishi ni suala ambalo linahitaji ulinganifu wa athari. Hivyo, mfasiri lazima

azingatie ulinganifu wa athari uliyopo katika matini chanzi na kuhawilisha kama ulivyo katika matini lengwa.

MAREJELEO

- BAKITA (2015) *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn.
- Hussein, E.M (1969a) *Kinjikitile*. Nairobi: Oxford University Press.
- Hussein, E.M (1969b) *Kinjikitile*. Nairobi: Oxford University Press.
- Massamba, D.P.B (2009) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mohamed, S.A (1995) *Amezidi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mohamed, S.A (2012) *He's Far Too Much* (Weschler, S & Kimambo, N, Translators). Nairobi. Longhorn.
- Nyangeri, N.A (2016) Makosa ya Kiamali katika Kutafsiri Vihisishi. Katika Kioo cha Lugha: Juzuu na 16.
- Wamitila, K.W (2003) *Kamusi ya Tashbihi, Vitendawili, Milio na Mishangao*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- TUKI (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.